



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MOMBA**



25.6.2021

**TANGAZO LA ZABUNI YA MAFUNDI WA UJENZI HOSPITALI
YA WILAYA MOMBA**

ZABUNI NO: LGA/142/2020-2021/NC/05

1. Halmashauri ya Wilaya ya Momba inawatangazia wananchi wote wenye sifa za ufundi wa ujenzi wa majengo kuwa inahitaji mafundi kwa ajili ya kazi ya kujenga Hospital ya Wilaya Momba.
2. Anakaribishwa Mtu binafsi au Kikundi kuleta maombi ya kazi ya ufundi wa ujenzi. Ujenzi huu utafanyika Kijiji cha Tindingoma Kata ya Chitete Wilaya ya Momba.

SEHEMU II: MAELEZO YA MAHITAJI

Maelezo Kazi	Namba ya Zabuni	Kazi Husika	Eneo la Ujenzi
Ujenzi wa Hospitari ya wilaya Momba	LGA/142./2020/2021/NC/05	Lot 01 Jengo la wagonjwa wa nje (OPD)	Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Momba Kijiji cha Tindingoma Kata ya Chitete.
		Lot 02 Jengo la Maabara	
		Lot 03 Nyumba ya takataka (Incinerator house)	


Sifa za mwombaji

- a) Awe na uzoefu wa kujenga majengo ya serikali
- b) Awe na uwezo wa kusoma ramani/michoro na kuitafsiri
- c) Aambatanishe uzoefu wa kazi amewahi kujenga majengo mbalimbali
- d) Aambatanishe cheti cha ujenzi kutoka chuo kinachotambulika na serikali kinachohusiana na masuala ya ujenzi.
- e) Awe na uzoefu kuanzia miaka miwili katika kazi za ujenzi wa majengo
- f) Asiwe anadaiwa au mgogoro wowote na Halmashauri
- g) Mwombaji asiwe na mgongano wa maslahi na Halmashauri

3. Kitabu cha maombi kinapatikana katika Ofisi ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi. Maombi yote yawe na nakala halisi (original) **moja(1)** na **nakala kivuli (Copy) moja(1)** zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na kusainiwa zilizowekwa kwenye bahasha na kuandikwa “Maombi ya kazi ya Ufundi wa ujenzi wa Hospitari ya Wilaya Momba” Zabuni Na. LGA/142/2020/2021/NC/05 Lot Na...Jengo la...Maombi haya yawasilishwe kwa:

**KATIBU BODI YA ZABUNI,
HALMASHAURI YA WILAYA MOMBA,
S.L.P 273 MOMBA**

4. Siku ya mwisho ya kuwasilisha zabuni ni **Alhamis Tarehe 08/07/2021 Saa 04:00 Asubuhi**. Zabuni zote zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha, mbele ya wawakilishi wa wazabuni walioamua kuhudhuria katika kikao cha ufunguzi wa zabuni utakao fanyika **Halmashauri ya Wilaya Momba**.
5. Zabuni zitakazochelewa, sehemu ya zabuni, zabuni za kielektroniki, na zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguzi wa zabuni hazitafanyiwa tathmini.


Adrian Jungu
**MKURUGENZI WA HALMASHAURI (W)
MOMBA.**

